



COVID-19, pia inayojulikana kama virusi vya korona, inafanya watu waugue kote ulimwenguni. Mbali na kuvaa barakoa, kukaa umbali wa futi 6 na kunawa mikono, **chanjo ni njia muhimu katika kusaidia kupunguza kasi ya kuenea kwa COVID-19**. Chanjo husaidia mwili wako kupigana na virusi na kukuepusha na magonjwa. Watu wengi wakipata chanjo, tutaweza kumaliza janga la COVID-19 kwa kasi zaidi.

Yafuatayo ni mambo kadhaa ya kufahamu kuhusu chanjo za COVID-19:

1. Chanjo za COVID-19 zinafundisha mwili wako jinsi ya kupambana na virusi vinavyokufanya uugue.

Chanjo za COVID-19 hazitakupa ugonjwa. Chanjo hufanya mwili wako ufikirie kuwa una ugonjwa bila kuambukizwa nayo. Mfumo wa kinga, sehemu ya mwili wako inayopambana na magonjwa, hukabiliana na chanjo kwa kuunda kingamwili. Kingamwili ni protini za ugonjwa mahususi ambazo hupambana na virusi wakati zinapovitambua. Hakuna chanjo yoyote iliyopo inayoathiri au kuingiliana na DNA ya mtu.

2. Chunguzi zinaonyesha kuwa chanjo hizi ni salama na zenye ufanisi.

Zaidi ya watu 117,000 walishiriki katika majaribio ya kimatibabu kwa chanjo tatu zilizopo – zaidi ya watu 43,000 katika jaribio la kimatibabu la Pfizer-BioNTech, zaidi ya watu 30,000 katika jaribio la kimatibabu la Moderna na zaidi ya watu 44,000 katika jaribio la kimatibabu la Johnson & Johnson. Watu wengi tofauti, wakiwemo watu wazima wazee na watu ambao ni Weusi, Asilia na watu wa rangi, walijumuishwa katika majaribio ya kimatibabu. Chanjo zote tatu ni salama na zina ufanisi sawa katika kuzuia kulazwa hospitalini na kifo. Hiki ndicho kiwango cha kawaida kinachotumika kutathmini chanjo zingine kama vile chanjo dhidi ya mafua.

Chanjo zilipitia majaribio ya kimatibabu, zikaidhinishwa kwa matumizi ya dharura na Usimamizi wa Vyakula na Dawa Marekani na zimependekezwa na wataalamu wa matibabu na afya ya umma kitaifa na hapa Vermont. Wakati mwingine, wakati chanjo inahitajika haraka, kama chanjo za COVID-19, watafiti wanachanganya hatua ili kuharakisha mchakato wa idhini. Hii haimaanishi kwamba wanaruka hatua zozote muhimu, lakini inasaidia mchakato kusonga mbele haraka zaidi.

Viungo katika chanjo za COVID-19 vinafanana na vile vinavyopatikana katika chanjo zingine. Zinajumuisha protini, mafuta, chumvi na michanganyiko ya kugandisha (polysorbate). Chanjo za mRNA (Pfizer-BioNTech na Moderna) pia zinajumuisha sukari na poliethilini glikoli (polyethylene glycol). **Hazijumuishi** tishu yoyote ya kijusi, bidhaa za nguruwe, mayai, jelatini, ulimbo wa mpira au dawa za kuzuia kuoza ndani yake.

3. Chanjo hizo zilitengenezwa baada ya utafiti wa miongo kadhaa.

Ingawa virusi mahususi vya korona vinavyosababisha COVID-19 ni vipya, wanasayansi wamekuwa wakichunguza chanjo za virusi vingine vya korona kwa miongo kadhaa. Utafiti wa chanjo za virusi vya korona ulianza mnamo mwaka wa 2003 wakati wa janga kali la Ugonjwa Mkali Sana wa Kupumua (SARS) na uliendelea mnamo mwaka wa 2012 wakati wa janga la Ugonjwa wa Kupumua wa Mashariki ya Kati (MERS). Wakati COVID-19 ilipotambuliwa, lengo la ulimwengu la kuondoa virusi hivi vipya vya korona, pamoja na ufadhili mwingi, zilisaidia kuharakisha mchakato wa utafiti ili kuunda chanjo salama na yenye ufanisi.

4. Chanjo ya COVID-19 inatolewa kwa dozi moja au mbili kulingana na aina ya chanjo.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ni ya dozi mbili, ya pili inatolewa siku 21 baada ya kwanza. Chanjo ya Moderna ni ya dozi mbili, ya pili inatolewa siku 28 baada ya kwanza. Chanjo ya Johnson & Johnson ni ya dozi moja. Zote tatu huchukua siku 14 kabla mwili wako uweze kupambana kwa ufanisi na virusi vinavyosababisha COVID-19.

5. Athari zinamaanisha chanjo inafanya kazi.

Baadhi ya washiriki katika majaribio ya kimatibabu kwa chanjo zote walionyesha mwitikio mkali wa kinga ambao mara nyingi husababisha baadhi ya athari. Kwa chanjo za dozi mbili, dozi ya pili inaweza kusababisha mwitikio ulio na kinga yenye nguvu zaidi kuliko dozi ya kwanza, jambo ambalo linaweza kusababisha athari zaidi. Hii ni kawaida na ndivyo mwili wako unavyojifunza kupambana na COVID-19. Athari nne zilizoonekana sana zilikuwa maumivu kwenye eneo lililodungwa sindano, uchovu, maumivu ya kichwa na maumivu ya misuli. Athari hizi zinapaswa kuondoka baada ya siku chache. Baadhi ya watu wamekuwa na athari za mzio kwa chanjo, lakini hii ni nadra sana.

6. Watu wengi walio na matatizo ya kimatibabu pia wanapaswa kupata chanjo.

Katika chunguzi za kimatibabu, chanjo za COVID-19 zilikuwa na ufanisi sawa kwa watu wasio na matatizo na walio na matatizo. Kwa kweli, watu walio na baadhi ya matatizo wana uwezekano wa kuugua sana ikiwa wanapata COVID-19, kwa hivyo hatua ya kupata chanjo inaweza kuwa muhimu hata zaidi. Ikiwa huna uhakika iwapo unapaswa kupata chanjo, zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu matatizo yoyote ya kiafya uliyonayo. Ikiwa huna mtoa huduma ya afya, piga simu kwa 2-1-1 ili uunganishwe na kliniki iliyo karibu nawe.

7. Unahitaji kuendelea kuchukua hatua za kuzuia COVID-19 baada ya kupata chanjo.

Inachukua muda kwa chanjo kufundisha mwili wako jinsi ya kupambana na COVID-19, kwa hivyo huwezi kulindwa na chanjo hadi wiki chache baada ya kupata dozi zote za aina ya chanjo unayopokea. Bado haijulikani ikiwa unaweza kusambaza virusi bila kujua baada ya kupata chanjo. Mpaka watu wa kutosha wapate chanjo na tupate maelezo zaidi, tunahitaji kufuata miongozo ya usalama kama vile kuvaa barakoa, kudumisha umbali wa futi 6 na kunawa

mikono, haswa karibu na watu ambao hawajapata chanjo au watu walio katika hatari kubwa ya kuugua sana kutokana na COVID-19.

8. Unaweza kujua iwapo unastahiki chanjo sasa, na mahali pa kupata wakati unapostahiki.

Tovuti ya Idara ya Afya ina maelezo kuhusu ni nani anayestahiki chanjo ya COVID-19, na ni nani atakayestahiki baadaye. Wakati unastahiki, utaweza kuweka miadi ya kupata chanjo. Tutaweka taarifa kwenye tovuti yetu, kwenye mitandao ya kijamii, na kwenye vyombo vya habari.

9. Chanjo za COVID-19 hazilipishwi..

Chanjo za COVID-19 hutolewa kwa Wanavermont bila gharama yoyote, hata ikiwa huna bima ya afya. Mtoa huduma anayekupa chanjo yako anaweza kutoza ada ya usimamizi kutoka kwa bima yako, lakini umehakikishiwa chanjo ya COVID-19 bila kulipa ada.

Pata maelezo zaidi katika [healthvermont.gov/COVID19vaccine](https://www.healthvermont.gov/COVID19vaccine)